

HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Maswa)

NEW

Telegrams: "MSW"
Telephone: 028 2750271
Fax: 028 2750376
E-mail: ded@maswadc.go.tz



S.L.P 170,
MASWA,
SIMIYU.

10.01.2019

Kumb.Na.MDC/ADM/10/30.VOL.I/54

TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Maswa anawatangazia wananchi wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya wilaya ya Maswa nafasi za kazi kama ifuatavyo:

1. Dereva Daraja la II – Nafasi 1

(a) Sifa za Mwombaji:

- (i) Awe na elimu ya kidato cha IV au VI
- (ii) Awe na leseni daraja la "C"
- (iii) Awe na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mitatu bila kusababisha ajali
- (iv) Awe na umri usiozidi miaka 45
- (v) Awe na cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II
- (vi) Awe na cheti cha kuzaliwa

(b) Mshahara: Ngazi ya TGS B sawa na Tsh.390,000 kwa mwezi.

2. Mtendaji wa Kijiji Daraja la II – Nafasi 3

(b) Sifa za Mwombaji

- (i) Awe na elimu ya kidato cha IV au VI
- (ii) Awe na Stashahada (Diploma) katika moja ya fani zifuatazo:
 - Utawala
 - Sheria
 - Elimu ya Jamii
 - Usimamizi wa fedha
 - Maendeleo ya Jamii au
 - Sayansi ya Jamii kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali
- (iii) Awe na umri usiozidi miaka 45
- (iv) Awe na cheti cha kuzaliwa

b) Mshahara: Ngazi ya TGS C sawa na Sh. 538,000 kwa mwezi.

Muhimu: Barua za maombi ziambatanishwe na nakala za vyeti vya Elimu, Taaluma na cheti cha kuzaliwa.

Maombi yote yatumwe kwa:

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya wilaya ya Maswa,
S.L.P 170,
Maswa –Simiyu.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 30.01.2019 saa 9.30 alasiri.

Robert E. Urassa
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA.